



Habari kwa wazazi wa shule za Chekechea

Kabla ya shule za chekechea zifungwe nchini Norway, hakujapatikana kuenea kwa maambukizi kati ya watoto wa chekechea. Ikilinganishwa na watu wazima, watoto wachache wamegundulika kama wameambukizwa nchini Norway na ulimwengu wote.

Shule za chekechea zitafunguliwa tena Jumanne, Aprili tarehe 21. Ili kukidhi mahitaji ya msimamizi wa kuzuia maambukizi, tumeona ni muhimu kupunguza masaa ya ufunguzi. Masaa ya ufunguzi yatakuwa kutoka saa mbili dakika kumi natano asubuhi hadi saa tisa mchana (08.15 - 15.00). Kwa wazazi walio katika fani muhimu za kijamii, kutakuwa na uwezekano wa kuongeza masaa ya ufunguzi kutoka saa moja na nusu asubuhi hadi saa tisa na nusu mchana (07.30 - 15.30) ikiwa utunzaji wa watoto hauwezi kupangwa vinginevyo. Wasiliana na bodi ya wakurugenzi katika shule ya chekechea..

Ni salama kwa watoto kwenda shule ya chekechea

Kupunguza maambukizi, tumeanzia hatua kadhaa katika shule za chekechea, na tutakuwa waangalifu zaidi kuhakikisha udhibiti mzuri wa maambukizi. Hii inategemea sisi wote tukifanya bidii na kufuata ushauri huo mpya. Katika chekechea, tutafanya yafuatayo:

- Osha mikono na kufuata watoto ili waweze kujifunza utaratibu mzuri wa kuosha mikono
- Kuwa na usafishaji mzuri katika shule za chekechea. Hatua mpya zilizo na orodha ya ukaguzi zimetayarishwa
- Osha vichezeo vya watoto baada ya kufunga shule kila siku
- Tumia wakati zaidi inje na watoto
- Kuwa na vikundi vidogo vya watoto (watatu wadogo / wasita wakubwa) ambao wako na wafanyikazi wa kudumu. Kutakuwa na barua tofauti kutoka kwa shule ya chekechea kuhusu mtoto wako anapaswa kuwa wa kikundi gani na mfanyakazi gani. Vikundi viwili vinaweza kuusiliana pamoja
- Kuwapa wafanyikazi mafunzo mazuri katika udhibiti wa maambukizo na mifumo / hatua zipya ambazo zimetayarishwa

Chakula katika chekechea

Msimamizi wa kudhibiti maambukizo anasema itakuwa utaratibu mzuri wa milo na kwamba chakula kitasambazwa kwa idadi ndogo. Tutatatia hivi:

- Watoto lazima wale chakula cha asubuhi nyumbani kabla ya kuenda shule ya chekechea
- Boksi au sanduku la chakula cha mchana lazima kiletwe shuleni pamoja na mwanafunzi,. Sanduku la chakula linawekwe kwenye rafu ya Wadi ya mtoto
- Chekechea hupanga chakula cha matunda kwa kumpa kila mtoto tunda mmoja



- Chekechea itagawa vinywaji kwa chakula cha mchana na matunda. Watoto hawapaswi kuleta chupa yao ya kunywa
- Chekechea itaandaa utaratibu wa kula

Kutakuwa na kupunguzwa kwa gharama za lische!

Chekechea bado itatoa utunzaji kwa watoto

Bado tutasimamia mahitaji ya utunzaji wa mwili kwa watoto na kuhakikisha watoto wote wanapata usalama, mahali na ustawi katika shule ya chekechea. Furaha na faraja bado ni muhimu kwa watoto, lakini itakuwa kwa wafanyikazi wa kawaida.

Ikiwa mtoto wako hajisikii vizuri

Ikiwa mtoto wako ana dalili za ugonjwa, pamoja na dalili nyepesi, hapaswi kuja chekechea. Dalili zinazoelezewa mara nyingi za covid-19 hapo mwanzo ni maumivu ya koo, homa na kukohoa kali, pamoja na kuhisi ugonjwa, maumivu ya kichwa na maumivu ya misuli. Maumivu ya tumbo yanaweza pia kutokea. Itakuwa muhimu sana watoto kubaki nyumbani kwa angalau siku moja baada ya kukosa dalili. Ikiwa mtoto anakuwa mgonjwa katika shule ya chekechea, lazima uchukue mtoto haraka iwezekanavyo.

Wazazi hawapaswi kuja kwa chekechea

Utapokea uandishi wako / mpango wako kutoka kwa chekechea kuhusu utoaji na uletaji wa mtoto shuleni. Lazima tugawane kwa vikundi ili kikundi kimoja kinaleta watoto ndani shuleni na kingine nje. Ikiwa imepangwa kuwa mtoto wako atakabidhiwa nje siku moja, itabidi mtoto avae nguo kulingana na hali ya hewa nje. Ikiwa mtoto analetwa ndani ya shule na unaona kuwa tayari kuna zaidi ya watu katika kabati za watoto, itabidi usubiri nje hadi upate nafasi. Wazazi hawapaswi kuja kwa shule ikiwa sio lazima, lakini hapa tumezingatiwa kwa uzito na uhitaji la usalama wa mtoto.

Usiletee vichezo vya watoto kutoka nyumbani

Watoto hawapaswi kuleta vichezo vyawo kutoka nyumbani. Ikiwa mtoto wako ana kisesere chake cha kulala yani «Teddy bear» unaweza kuleta. Lakini ni muhimu zaidi kwamba haishirikiwi na watoto wengine katika chekechea.

Kuosha mikono ni muhimu nyumbani kama ilivyo katika shule ya chekechea. Osha mikono yako kabla ya kuja kwenye shule ya chekechea, na mara tu utakapofika nyumbani. Watoto wanapaswa pia kuosha mikono wanapokuja kwenye chekechea.

Nguo ambazo watoto hubeba katika chekechea lazima ziweke kwenye begi au gunia kwenye rafu ya mtoto kwenye kabati.

Nguo za watoto zinapaswa kuoshwa kwa digrii 60.

Tunapendekeza usome mwongozo wa kudhibiti maambukizi ulio kwenye wavuti ya udir.no:
<https://www.udir.no/kvalitet-og-kompetanse/sikkerhet-og-beredskap/informasjon-om-koronaviruset/smittevernveileder/barnehage/>

Ikiwa unamaswali, wasiliana na bodi ya wakurugenzi wa chekechea husika!

Kwa salamu,
Bente Ingebretsen
Msimamizi wa chekechea
Lyngdal kommune

